

SELF MF



**"Giving the
People a working
chance"**

SELF MICROFINANCE FUND

FOMU YA MAOMBI YA MKOPO WA MFANYAKAZI

Nimeambatanisha vifuatavyo

- Nakala iliyothibitishwa ya kitambulisho cha mfanyakazi.
- Stakabadhi za Mshahara za miezi mitatu ya mwisho (Salary slip).
- Barua yakuitwa kazini iliyothibitishwa na mwjiri.
- Barua ya kuthibitishwa kazini.
- Picha mbili ndogo za rangi
- Nakala ya mtiririko wa akaunti ya benki ya miezi mitatu (Bank Statement).

SEHEMU A: FOMU YA MAOMBI YA MKOPO

Tafadhali kamilisha fomu hii (kwa **HERUFI KUBWA**) halafu rudisha katika moja ya matawi yetu.

1. Taarifa binafsi za mkopaji

Jinsia - Weka alama ya Vema (V) Me Ke

Jina la kwanza	Jina la kati	Jina la ukoo
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
Tarehe ya kuzaliwa	Simu ya Nyumbani	Simu ya Mkononi
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
Barua Pepe	Namba ya Kitambulisho cha kazi	Namba ya Kitambulisho Kingine
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

2. Taarifa za Benki/ mikopo mingine

Benki/Taasisi	Tawi	Namba ya Akaunti	Kiasi cha mkopo	Rejesho kwa mwezi	Kiasi kilichobaki
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

3. Taarifa za Makazi

Mkoa /Jiji	Wilaya	Kata	Mtaa
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

Namba ya Nyumba	Namba Ya kiwanja	Nyumba Ya Kumilili	Nyumba ya Kupanga	Nyumba Ya Mwijiri	Nyumba ya wazazi /Ndugu/Rafiki
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

4. Taarifa za Ajira

Jina la mwajiri wa sasa	<input type="text"/>	Anuani	<input type="text"/>	Namba ya simu	<input type="text"/>
Kazi yako	<input type="text"/>	Ajira yakudumu	<input type="text"/>	Tarehe ya kustaafu	<input type="text"/>
Mshahara wako kwa mwezi	<input type="text"/>	Ajira ya Mkataba	<input type="text"/>	Mwisho wa mkataba	<input type="text"/>
Jina la mwajiri wa zamani	<input type="text"/>	Anuani	<input type="text"/>	Namba ya simu	<input type="text"/>
Kazi yako	<input type="text"/>	Muda uliofanyakazi	<input type="text"/>	Sababu za kuacha kazi	<input type="text"/>

5. Taarifa za mkopo

Naomba mkopo wa mshahara kutoka SELF Microfinance Fund

Kiasi cha mkopo	Muda wa mkopo
<input type="text"/>	<input type="text"/>

Dhumuni la mkopo (weka alama ya vema (v) panapostahili)

Ada ya shule Matibabu Kununua kiwanja Mengineyo

6. Wadhamini

Mimi _____, na Mimi _____, nimekubali kumdhamini Bw /
Bibi _____ kwa hiari yangu mwenyewe bila kushurutishwa na mtu yeyote na nikiwa naakili zangu timamu.
Endapo mkopaji atashindwa kulipa/ atahama eneo la makazi au kazi, nitawajibika kutoa ushirikiano kwa SELF MF kuhakikisha deni/
mkopo wote unalipwa.

	Mdhamini Wa Kwanza	Mdhamini wa Pili (<i>lazima awe ndugu/ mwenzu</i>)
Jina la Mdhamini		
Uhusiano		
Kazi		
Simu ya nyumbani/Ofisini		
Simu ya mkononi		
Anuani ya makazi		
Tarehe ya kuzaliwa		
Sahihi ya mdhamini		

Ulipataje taarifa ya kuwepo mikopo ya wafanyakazi ya SELF Microfinance Fund?

7. Tamshi/Tamko

- Nathibitisha kwamba taarifa hizi ni sahihi na za kweli na ninaidhinisha SELF Microfinance Fund kuwasiliana na yeyote kwa ajili ya uthibitisho.
Nina kubali kufungwa na masharti ya mkopo huu. Ninaelewa kuwa SELF Microfinance Fund ina haki ya kukataa maombi haya bila ya kutoa sababu.
- Mimi, mkopaji, nakubaliana na masharti yafuatayo (weka alama panapohusika)
 - Ninakubali kukatwa kiasi cha marejesho ya mkopo wangu kila mwezi na kuwasilisha kiasi hicho SELF Microfinance Fund kwa madhumuni ya kutimiza masharti ya ulipaji mzuri wamkopo.
- Ninamuidhinisha mwajiri wangu itokeapo kukoma kwa ajira yangu iwe kwa kuacha kwa hiari, kuacha ghafla, kufukuzwa, kupunguzwa au kusimamishwa kazi nitakuwa mwaminifu kuendelea kulipa deni la SELF Microfinance Fund na mafao yangu yaliyopo PSSSF/ NSSF naomba yatumike Kama malipo ya salio la mkopo.
- Mimi mkopaji, nakubali na kuidhinisha SELF Microfinance Fund:
 - Kufanya mauzo kwa benki, taasisi ya fedha au kitengo cha usimamizi mikopo vilivyoteuliwa na Shirikisho la Mabenki Tanzania au Benki Kuu kuthibitisha taarifa nilizotoa;
 - Kutafuta taarifa zinazonihusu kutoka kwa benki, taasisi ya fedha, au kitengo cha usimamizi mikopo vilivyo teuliwa na Shirikisho la Mabenki Tanzania na au Benki Kuu wakati wowote nifanyiwapo uchunguzi;
- Agano hili linatawaliwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jina la muombaji

Tarehe

Picha ya muombaji

Sahihi ya muombaji

Dole gumba

8. Uthibitisho waMwajiri

Mwajiri/Taasisi
Simu

Anuani
Tarehe

Pendekezo la Mkuu wa Idara/Kitengo/Afisa Utawala

<input type="text"/>	Mhuri
----------------------	-------

Jina
Sahihi

Cheo
Tarehe

Ridhaa ya Mwajiri/Afisa aliyeidhinishwa

<input type="text"/>	Mhuri
----------------------	-------

Jina
Sahihi

Cheo
Tarehe

SEHEMU YA 9: VIAMBATISHO

Kwa matumizi ya SELF Microfinance Fund tu:

Vitu muhimu vya kuthibishwa na afisa mikopo wa tawi

- Orodha ya viambatisho muhimu imekamilika
- Kuthibitisha makato ya muombaji yameingizwa kwenye mfumo (Lawson)
- Fomu ya mwombaji iliyo thibitishwa na muajiri

Pendekezo la afisa mikopo:

Kiasi cha Mkopo	Jina	Sahihi	Tarehe
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

Meneja wa tawi:

Kiasi cha kilichodhibitishwa	Jina na sahihi	Tarehe
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>
Kiwango Cha Riba	Kipindi Cha Kulipa (Miezi)	Makato ya kila mwezi
<input type="text"/>	<input type="text"/>	<input type="text"/>

Kupitisha Mkopo (Umepitishwa/ Umekataliwa)

Cheo	CMM	DCO	DCS	DBD	HLS	CEO
Sahihi						
Tarehe						

SEHEMU B: MKATABA WA MKOPO

Mkataba huu wa mkopo umefanyika leo tarehe _____ ya mwezi wa _____ Mwaka _____

KATI YA

SELF Microfinance Fund ya S.L.P 77760, Dar-es-Salaam (Atakayejulikana kama mkopeshaji; pamoja na mwakilishi wake na mtu ye yote atakayepewa dhamana na mkopeshaji); kwa upande mmoja.

NA

Bw/Bi. _____ wa _____ S.L.P _____, -
_____, anayefanya kazi katika kampuni/shirika/taasisi/wizara _____
(Atakayejulikana kama Mkopaji; pamoja na mwakilishi wake na mtu ye yote atakayepewa dhamana na mkopaji); kwa upande mwingine.

MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO: -

1. KWAMBA, kulingana na mkataba huu mkopeshaji amekubali kumkopesha mkopaji mnamo tarehe _____ 2020 (“Tarehe ya mkopo”) Jumla ya Shilingi _____ -
_____ (Tshs _____/=);
2. Mkopo huu utatozwa riba ya asilimia 16% kwa mwaka. Mkopeshaji ana haki ya kubadili riba kutokana na sababu za kiuchumi na viwango vilivyo katika soko.
3. Mkopo huu pia utatozwa ada ya mkopo ya asilimia mbili (2%) ya kiasi cha mkopo ulioidhinishwa. Ada hii hulipwa maramoja na hairudishwi;
4. Mkopo huu utatozwa bima ya mkopo ya asilimia sifuri nukta sita (0.6%) ya kiasi cha mkopo ulioidhinishwa kwa Mwaka;
5. Mkopaji anamruhusu mwajiri wake kukata malipo ya kila mwezi na kuyawasilisha SELF Microfinance Fund kwa dhumuni la kulipa mkopo huu kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la marejesho liloambatanishwa;
6. Kulipa mkopo wote kwa mkupuo mapema inaruhusiwa.
7. Kama masharti yaurejeshaji Mkopo yatafunjwa na Mkopaji, faini ya asilimia tatu (3%) kwa mwaka ya kiasi cha mkopo ambao haujarejeshwa kitatozwa.
8. Mkopaji atalazimika kufuata na kutekeleza masharti na makubaliano ya mpango wa utekelezaji wa mikopo ya wafanyakazi baina ya SELF Microfinance Fund na kampuni iliyomwajiri.
9. Mkopeshaji anauwezo wa kukubali au kukataa maombi ya mkopo kwa uamuzi wake binafsi bila kutoa sababu ya kukubali au kukataa ombi.
10. Mkopaji anakubali kwamba Mkopeshaji anauwezo na haki ya kupandisha kiwango cha riba kutoka kiwango cha kawaida kilichotajwa katika kifungu cha 2 cha mkataba huu kwa mwaka endapo Mkopaji atapoteza ajira yake ya sasa kwa sababu yeyote ile;
11. Mkopaji anaahidi kutoa dhamana na kusaini nyaraka za kisheria kuhusu dhamana hizo kama ikitokea Mkopaji amapoteza kazi kwa mwajiri;
12. Mkopaji anawajibu kuhakikisha Mkopeshaji anataarifa ya mahali anapoishi baada ya kukoma kwa ajira yake kwa kipindi chote atakapokuwa bado ana deni na Mkopeshaji na anakubali kumjulisha Mkopeshaji ndani ya siku kumi (10) iwapo atabadili anuani kwa kuhama makazi;

13. Makubaliano tofauti na haya hayana nguvu yeyote isipokuwa kama makubaliano hayo yameandikwa na kutiwa saina na pande mbili husika wa makubaliano haya.
14. Kama kwa sababu yeyote iwayo ile sehemu ya makubaliano haya itaonekana kutokuwa ya ukweli na kutotimizwa basi sehemu hiyo itatengwa na kuangaliwa tofauti au kuondolewa inapobidi na haitoathiri sehemu iliyobaki ya makubaliano hayo.
15. Mkopaji anakubali kuwa endapo atashindwa kutimiza masharti ya makubaliano haya, Mkopeshaji anahaki ya kuchukua hatua zozote kuweza kufidia deni la mkopaji wa SELF Microfinance Fund katika zoezi hilo ikiwa ni pamoja na huduma za kisheria.
16. Migogoro au kasoro yeyote itakayotokea baina ya mkopaji na mkopeshaji itatatuliwa kwa njia ya mazungumzo na maelewano baina yao. Iwapo kutakuwa na kutokuelewana migogoro hiyo itatatuliwa kwa njia ya usuluhishi kufuata sheria ya Usuluhishi ya Tanzania (Arbitration Act).
17. Itokeapo kukiukwa kwa masharti haya naya nyaraka dhamana zilizoandaliwa, salio la mkopo pamoja na kiwango cha riba kitalazimika kulipwa wakati huo huo kama kukiuka huko kwa masharti hakutarekebisha ndani ya siku thelathini (30) baada ya SELF Microfinance Fund kumwarifu na kumtaka mkopaji kurekebisha ukiukwaji huo, na yafuatayo yanaweza kuwa vigezo vya kufikiwa kwa uamuzi huu:
 - I. Iwapo mkopaji atashindwa au kukiuka kulipa kwa viwango vya mwezi kama ilivyokubaliwa muda unapofika. Kwa dhumuni la sharti hili, kukiuka kulipa kutatambulika wakati kiwango cha mwezi hakijalipwa ndani ya siku thelathini (30).
 - II. Iwapo Mwajiri au Mkopaji watakiuka masharti yeyote katika dhamana ya Mwajiri iliyosainiwa na Mwajiri au,
 - III. Kusimamishwa kwa shughuli za utendaji au biashara kwa mwajiri au kugawanywa kwa mali zote kwa wanaomdai;
 - IV. Amri ya mahakama juu ya umiliki wa mali ya mkopaji au kama mkopaji atafanya chochote kusababisha Amri kama hii au;
 - V. Mkopaji atavunja au anajaribu kuvunja masharti na makubaliano au;
 - VI. Makubaliano hayo yanapofikia kikomo au;
 - VII. Mkopaji anapofungwa kwa Zaidi ya mwaka mmoja.
18. Mkopaji anakubali kuidhinisha Mkopeshaji, taasisi ya fedha au taasisi ya usimamizi mikopo iliyoteuliwa na shirikisho la Mabenki Tanzania.
 - I. Kufanya maulizo kwa benki, taasisi ya usimamizi mikopo iliyoteuliwa na shirikisho la Mabenki Tanzania ili kuthibitisha taarifa zilizotolewa;
 - II. Kutafuta taarifa zinazonihusu kutoka kwa benki, taasisi ya fedha au taasisi ya usimamizi mikopo iliyoteuliwa na shirikisho la Mabenki Tanzania wakati wowote nifanyiwapo uchunguzi;
 - III. Kutoa taarifa zangu kuhusiana na mkopo nilionao kwa SELF Microfinance Fund kwa taasisi ya usimamizi mikopo iliyoteuliwa na Shirikisho la Mabenki Tanzania. Mkopaji anatambua na anakubali wamba ametia saina fomu hii ya maombi kama ishara ya kwamba amekubaliana na masharti yake.
19. Mkataba huu na vielelezo vingine ambavyo vinahusiana na mkataba huu mathalani fomu ya kuombea mkopo, barua za wadhamini, na makubaliano ya mpango wa utekelezaji wa mikopo ya wafanyakazi vitakuwa na kutafsiriwa kama sehemu ya mkataba huu.
20. Mkataba huu wa Mkopo, haki na Majukumu ya pande zote mbili yataendeshwa na kutawaliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

INASHUHUDIWA KWAMBA, PANDE HUSIKA ZIMESAINI MKATABA KAMA ILIVYOAINISHWA HAPO JUU.

IMESAINIWA NA

JINA:

Leo.....mwezi..... 2020



.....

MKOPAJI

IMESAINIWA KWA NIABA YA SELF MCFINANCE FUND NA

JINA:

Leo.....mwezi..... 2020



.....

MKOPESHAJI